MAMLAKA YA MAENDELEO YA BIASHARA TANZANIA



## PROGRAMU YA UWEZESHAJI WAFANYABIASHARA SEKTA YA NYUKI NA MAZAO YAKE



*Picha ya pamoja ya Wahitimu wa Mafunzo ya uwezeshaji biashara mazao ya nyuki Mkoani Tabora. Waliokaa katikati ni Mkuu wa Chuo cha Nyuki Tabora (BTI)*

**Utangulizi**

Tanzania ni moja ya nchi zenye wazalishaji wa asali tokea enzi za kale. Asali inatokana na nyuki wanaodunga na wasiodunga kutoka kwenye mizinga ya jadi ya magome ya miti, magogo na majani yaliyosukwa na kutundikwa. Kukua kwa utaalamu na maarifa kumewezesha Watanzania kubadili ufugaji nyuki kutoka hali ya kijadi na kuwa katika ufugaji wa kibiashara. Ufugaji nyuki kisasa umeongeza tija katika urinaji, ubora wa bidhaa na idadi ya mazao ya nyuki. Kwa hivi sasa mazao ya nyuki yanayotambulika na kufanyiwa kazi ni pamoja na Asali, Nta, Gundi, Chavuo, Sumu ya Nyuki na Maziwa ya Nyuki. Mazao haya yanaifanya sekta kuwa na fursa kubwa ya biashara na uwekezaji katika kuendeleza bidhaa, zana za ufugaji nyuki na urinaji wa asali, uchakataji na ufungashaji wa asali na mazao mengine ya nyuki.

### Uzalishaji wa Mazao ya Nyuki

Tanzania ni nchi yenye fursa ya ufugaji nyuki kwa kuwa na misitu ya asili yenye ukubwa wa hekta milioni 48 pamoja na mashamba yenye uoto wenye kutoa maua kwa misimu ya kilimo. Sehemu kubwa ya Wafugaji nyuki Tanzania hurina asali kwa misimu miwili au mitatu kutegemeana na msimu wa maua mengi, mazingira na aina ya mizinga. Mrejesho wa mafunzo unaonesha uzalishaji wa mazao ya nyuki unongezeka kutokana na kujengewa ufahamu namna ya kuendesha manzuki kibiashara kwa washiriki wa mafunzo mwaka 2016 na 2017 kutokana na uvunaji mara mbili kwa mwaka na uzingatiaji wa viashiria vya muda wa kalenda ya mpangokazi katika manzuki.

### Uwezeshaji Sekta ya Nyuki na Mazao Yake

TanTrade inashirikiana na Taasisi nyingine katika kutoa mafunzo ya kujenga uelewa wa namna ya kuwekeza katika sekta ya ufugaji nyuki kibiashara. Washiriki walipata elimu ya uendeshaji na usimamizi wa manzuki kibiashara ili kujenga nguvu ya ushindani katika masoko ya ndani na nje. Mpaka kufikia Machi, 2018 jumla ya washiriki 602 wahihudhuria na kati ya hao wanawake walikuwa 122 kutoka mikoa tisa.

Katika mafunzo hayo, TanTrade ilishirikiana na Taasisi za Umma na Binafsi zilizopo kwenye maeneo husika. Taasisi hizo ni BTI, CHEMA, NCAA, TBS, TFDA, TFS, TIRDO, SIDO, na SYECCOS, Ofisi za Mkoa na Halmashauri za Wilaya katika uratibu wa washiriki.

### Programu za Uwezeshaji Mafunzo

Programu hii ilianza baada ya utafiti wa mahitaji ya ushindani wa bidhaa katika soko kwa mazao ya nyuki uliofanyika katika Mikoa ya Kagera, Singida, Geita na Shinyanga. Mafunzo haya yamekwisha tekelezwa kwa washiriki wa Mikoa ya Singida, Tabora, Katavi, Arusha, Kagera, Shinyanga, Kigoma, Mwanza, Simiyu ambapo jumla ya washiriki 602 ambao ni wafugaji na wafanyabiashara wa mazao ya nyuki.

**Programu ilihusisha mafunzo ya:**

- Programu ya mafunzo;
- Ufugaji bora wa nyuki na manzuki;
- Uongezaji wa makundi ya nyuki;
- Zana na vifaa vya uwekezaji manzuki;
- Ubora na viwango katika asali na Nta;
- Soko katika mnyororo wa thamani wa asali na mkakati wa kufikia soko;
- Mnyororo wa ufuatiliaji na uthibiti ubora;
- Uchakataji na ufugashaji asali;
- Usalama wa bidhaa na mazingira ya uzalishaji;
- Uendeshaji wa biashara ya mazao ya nyuki (asali na nta); na
- Ushiriki wa maonesho ya biashara.

## Matukio ya Mafunzo



*Washiriki wa mafunzo kwa vitendo wakiwasha mshumaa baada ya kuutengeneza Mkoani Singida.*



*Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa TanTrade akitoa hotuba kwa washiriki wakati wa ufunguzi wa mafunzo Mkoani Tabora.*



*Zana na vifaa vya ufugaji na uchakataji wa mazao ya nyuki wakati wa mafunzo Mkoani Tabora.*



*Mkufunzi kutoka SIDO Tabora akitoa mada ya kuweka lebo katika kifungashio cha asali.*

## Soko la Asali

Sehemu kubwa ya asali inayozalishwa inauzwa hapa nchini na kiasi kidogo kinauzwa nje ya nchi. Nchi hizo ni pamona na Germany, Oman, Belgium, Japan, United Kingdom, South Africa, Uganda, Hong Kong, Italy, , Jamaica, South Korea, Netherland, Norway, Quarter, Russian Federation, Kenya, Rwanda, China, Saudi Arabia, Seychelles, Sweden, UAE, USA DRC na Mozambique

Katika soko la kimataifa fursa kubwa ya mazao ya nyuki ipo soko la ulaya na kufuatiwa na marekani. Katika soko la Ulaya ni nchi sita ambazo ni Ujeruani (15%), Ufaransa (6.4%), Belgium (3.8%), Italy (3.9%) na Spain (3.1%) nyingine ni UK (6.2%), Japan (6.4) na China (3.0%). Manunuzi ya asali soko la dunia kwa mujibu wa tafiti za Technavio, Jesse Maida imeeleza kuwa yataongezeka tani milioni 6.2 mwaka 2016 hadi kufikia tani 8.1 mwaka 2021. Mauzo hayo katika soko la kimataifa mwaka 2017 yaliuzwa kwa tani kati ya Shilingi milioni 3.83 hadi Shilingi milioni 19.68 kwa fob kulingana na Nchi inakotoka.

TanTrade inawezesha wafanyabiashara wa mazao ya nyuki kwa kutenga *banda maalumu la asali* wakati wa Maonesho ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam pamoja na kuandaa siku *maalumu ya asali* inayoadhimishwa kila Maonesho ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam na kukutanishwa na wanunuzi wa ndani na nje ya nchi kwenye mikutano ya wafanyabiashara ya ana kwa ana.

Aidha, maonesho ya kipekee ya sekta ya nyuki na mazao yake yalifanyika Oktoba 2012 katika Uwanja wa Maonesho ya Biashara wa Mwl. J. K. Nyerere Dar es Salaam na Maonesho mengine sambamba na Apimondia yalikuwa Novemba, 2014 Mkoani Arusha. Matukio hayo yalitoa mwelekeo na mtazamo wa pekee katika kuendeleza Sekta ya Nyuki Nchini. Mikakati hiyo itaendelezwa ili kuongeza uzalishaji na utumiaji wa asali kwa ustawi na afya ya jamii kwa ujumla.



***"TanTrade kwa Ukuzaji wa Biashara"***


**Mkurungenzi Mkuu,**
Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania,
S. L. P 5402, **Dar es Salaam.** Tanzania
Tovuti: www.tantrade.go.tz
Barua pepe:info@tantrade.go.tz
Simu: +255 22 2850238 / 2850065